



Hadithi ya Malik

-  LIDA Italia
-  Vilius Aistis Vilimas
-  Jacob Haule
-  4
-  Kiswahili SW



Jina langu ni Malik na nina umri wa miaka 39.
Nilizaliwa huko Afghanistan. Dini yangu ni tofauti na
dini kuu ya Afghanistan.



Kwa miaka mingi, watu wa dini yangu wamekuwa wakiteswa. Hii imekuwa ni changamoto kubwa sana kwa familia yangu.



Miaka michache iliyopita kulikuwa na vita. Nilikuwa na hofu kwamba ningeuwawa. Niliacha familia yangu na kwenda Ulaya na kuanza maisha mapya.



Nilitembea kwa kilomita nyingi na wakati mwingine sikuwa na chakula wala sehemu ya kukaa. Baadhi ya watu niliosafiri nao walifariki.



Hatimaye nilifika Ulaya. Nilikutana na watu kutoka kwenye nchi yangu ambao walinisaidia. Sifahamu ningelifanya nini bila wao.



Nilianza kujifunza lugha, lakini ilikuwa ngumu. Nilijua kwamba kuongea lugha hiyo ilikuwa muhimu katika kupata kazi.



Nilijifunza kwa miaka kadhaa, cha kwanza kabisa ni kujifunza lugha. Ilikuwa ngumu, lakini ninafurahi kujifunza mambo mapya.



Baada ya kujifunza, nikaanza kufanya kazi. Kwanza nilifanya kazi katika mgahawa, na kisha nikawa mwalimu kwa sababu ninataka kusaidia wengine.



Ninatumaini kuwa siku moja nitarejea Afghanistan.
Watu wengi huko wanahitaji msaada na ninataka
kuwasaidia.




LIDA Stories

lidastories.net

Hadithi ya Malik

 LIDA Italia

 Vilius Aistis Vilimas

 Jacob Haule

